# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

## MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU WA ELIMU YA MSINGI NGAZI YA CHETI

## HISTORIA

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2009

ISBN

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa, kunakili au kuchapisha kwa namna yoyote muhtasari huu bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Imebuniwa na kutayarishwa na

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar -es- Salaam
Tanzania

Simu: +255 222 773005, 2774420
Nakushi: +255 222 774420
Barua pepe: director.tie@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

## IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu wa |Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti Historia wa mwaka 2009.**

**Umeidhinishwa na ……………………………………….**

**Saini …………………………………………………………**

**Tarehe …………………………………………………. 2009**

**Kamishna wa Elimu**
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S.L.P. 9121
**DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 222 110150, 1101799, 11046**
**Nukushi: + 255 222 11 3271**
**Wovuti: www.moe.go.tz**

## YALIYOMO

**Ukurasa**


Utangulizi … … … … … …. … … … v
Maelezo kuhusu muhtasari … … … … …. … …. … v
Sababu za kuwa na muhtasari … …. … … … … … … vi
Madhumuni ya kufundisha somo la Historia … … … … … … vi
Ujuzi wa somo … …. …. …. …. …. …. …. …. …. vi
Malengo ya somo …. … …. …. …. …. …. …. …. …. vi
Muundo wa muhtasari… …. … … … … … …. … vii
Muda wa Mafunzo…. …. …. …. …. …. …. …. …. …. …. vii
Upimaji…. …. …. …. …. …. …. …. …. …. …. …. …. vii

**SEHEMU YA KWANZA: TAALUMA**

Madhumuni ya kufundisha Taaluma ya somo la Historia … … … … … … 1
Ujuzi katika Taaluma ……………… … …. … … … 1
Malengo ya kufundisha Taaluma …………………. …………..….…… 1
1.0 Ukoo wetu … …. … … … … … … 3
2.0 Chuo chetu … …. … … … … … … 5
3.0 Asili na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia na Mazingira … … 6
4.0 Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika .. 9
5.0 Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Afrika … …. … 11
6.0 Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika … … … … 12
7.0 Ukombozi wa Bara la Afrika … …. … … … … 13
8.0 Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru … 15
9.0 Ushirikiano wa Kimataifa … …. … … … … 17

**SEHEMU YA PILI: UFUNDISHAJI**

Madhumuni ya Kufundisha Ufundishaji wa Somo la Historia … … 21
Malengo ya Kufundisha Ufundishaji wa Somo la Historia … …. … 21
Ujuzi katika Kufundisha Ufundishaji wa Somo la Historia … …. … 21
1.0 Misingi ya Ufundishaji/Ujifunzaji wa Somo la Historia ... … 23
2.0 Uchambuzi wa Vifaa/Zana za Kufundishia/Kujifunzia … … … 25

3.0 Kujiandaa kwa ajili ya Kufundisha … …. … … … 27
4.0 Ufundishaji wa Maudhui ya Somo la Historia … …. … … 33
5.0 Upimaji na Tathmini … …. … … … …. … 35
Rejea … …. … … … …. … … … … 38

# Utangulizi

## Maelezo kuhusu Muhtasari

Muhtasari huu wa Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti, somo la Historia, unachukua sehemu ya nafasi ya *Muhtasari wa Mbinu za Ufundishaji wa Maarifa ya Jamii (2000)* ambao ulichapishwa 2003. Kuanzia 1998 serikali ilisitisha ufundishaji wa somo la Historia katika shule za msingi na badala yake kukawa na somo la Maarifa ya Jamii. Kufuatia uamuzi huo somo la Historia (Taaluma na Ufundishaji) halikufundishwa katika mtaala wa mafunzo ya ualimu daraja A (sasa Ngazi ya Cheti) kuanzia 1999. Badala yake lilianza kufundishwa somo la Mbinu za Kufundisha Maarifa ya Jamii na kuacha kabisa kufundisha taaluma ya Historia.

## Sababu za kuwa na Muhtasari

Somo la Historia lilikuwa likifundishwa katika vyuo vya ualimu daraja C na B (ambayo sasa yamefutwa) na pia katika Daraja A hadi mwaka 1998. Baada ya mwaka 1998 somo lilifundishwa kama Maarifa ya Jamii ambalo lilikuwa ni somo lililounganisha masomo ya Historia, Uraia na Jografia. Kuanzia mwaka 2006 masomo hayo yalirudishwa tena na kuwa masomo yanayojitegemea.

Pia, ufundishaji katika vyuo vya ualimu ulikuwa unazingatia taaluma na ufundishaji hadi mwaka 2000, ambapo yalifanyika mabadiliko na mkazo ukawekwa katika mbinu za ufundishaji tu.

Katika kipindi hicho, msisitizo umekuwa kwenye mbinu za kujifunzia na kufundishia tu. Baada ya utekelezaji wake, ilibainika kwamba wakufunzi na wanachuo wanahitaji pia kupata stadi zaidi katika eneo la taaluma ya somo. Hivyo basi mwaka 2009 iliamuliwa kuwa somo la Historia lifundishwe kwa kuzingatia Taaluma na Ufundishaji.

Mabadiliko haya yalilenga kumwezesha mkufunzi kumudu ufundishaji wa somo kwa kuzingatia Taaluma na Ufundishaji/Ujifunzaji wake.

Muhtasari huu unalenga kukidhi haja ya kuwa na walimu na wakufunzi wenye uwezo wa kumudu Taaluma, maudhui na ufundishaji wa somo la Historia.

**Madhumuni ya kufundisha somo la Historia.**

a) Kuwawezesha wanachuo wapate na wajijengee uwezo wa kumudu somo la Historia
b) Kuwawezesha wanachuo kuinua kiwango chao cha kuthamini utamaduni, mila na desturi za Mtanzania.
c) Kuandaa waalimu wenye stadi na mbinu za udadisi, utafiti, ufahamu na kuheshimu utu na haki za binadamu.

**Ujuzi wa somo**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili (2) Mwanachuo awe na uwezo wa:

a) Kubaini, kushauri na kunasihi wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali na maalum kwa kuzingatia mazingira jumuishi.
b) Kukuza maendeleo ya kihaiba, kiakili na tabia za kimaumbile kwa wanafunzi wa shule za Msingi.
c) Kutumia Stadi mbalimbali, Maarifa ya Kiteknolojia na ubunifu katika ufundishaji.
d) Kupima na kutathmini maendeleo ya Wanafunzi kitaaluma na kitabia.
e) Kutumia Stadi za Kiuongozi na Kiutawala kuweka ulinzi na usalama kwa wanafunzi wa shule za Msingi.
f) Kufanya tafiti ndogo ndogo kuhusu maendeleo ya wanafunzi katika kujifunza.
g) Kubuni, kutengeneza na kutumia zana katika kufundisha na kujifunza.
h) Kutafuta maarifa na stadi katika kujiendeleza kitaalam.
i) Kumudu maudhui ya mada za masomo atakayofundisha.
j) Kubainisha, kutafsiri na kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuko
k) kutumia lugha ya kufundishia kwa ufasaha .

**Malengo ya somo**

**Baada ya mafunzo ya miaka miwili (2) mwanachuo aweze:-**

a) Kukuza uelewa wa Wanachuo katika nadharia za kielimu, Kanuni, Utafiti, Misingi ya Mitaala na utendaji.
b) Kuendeleza uwezo wa mwanachuo kuweza kumudu masomo ya taaluma, ufundishaji, teknolojia na ubunifu.
c) Kumwezesha mwanachuo kukuza mbinu za kusimamia uongozi na utawala wa darasa .

c) Kutoa nafasi kwa wanachuo kuweza kujiongezea maarifa na ujuzi katika ushauri nasaha, elimu maalum na masuala mtambuko.
d) Kuandaa walimu wenye stadi na mbinu za utafiti, upimaji na tathmini.
e) Kufanya upimaji wa wanafunzi, kuweka kumbukumbu za matokeo ya kazi za wanafunzi na kutoa taarifa za maendeleo yao kwa wadau husika.

**Muundo na Mpangilio wa Muhtasari**

Muhtasari huu wa Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti, una sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Taaluma ya Historia. Sehemu ya pili ni Ufundishaji wa Historia. Mwanzoni kuna utangulizi unaofuatiwa na sababu ya kuutunga na maelezo ya mpangilio wa vipengele vya muhtasari.

Sehemu A, yaani Taaluma ya Historia, inaanza kwa kubainisha madhumuni ya kufundisha taaluma ya Historia. Hii inafuatiwa na malengo ya taaluma inayofundishwa, na ujuzi unaotakiwa kukuzwa kwa wanachuo. Kinachofuata ni mada kuu 9 zenye jumla ya mada ndogo 24. Mwisho kuna orodha ya rejea. Hivi ni vitabu na maandiko yaliyorejewa wakati wa kuandika muhtasari na ambayo mkufunzi anashauriwa kuyasoma.

Sehemu B, yaani Ufundishaji wa Historia, pia inaanza kwa kubainisha madhumuni ya kufundisha ufundishaji wa Historia. Hii inafuatiwa na malengo ya kufundisha ufundishaji pamoja na ujuzi unaotarajiwa kukuzwa kwa mwanachuo. Baada ya vipengele hivyo kuna mada kuu 5 zenye mada ndogo 17. Mwishoni kuna orodha ya rejea.

**Muda wa Mafunzo**

Muda wa mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni miaka 2. Somo la Historia lina vipindi 2 kwa wiki na muda wa kila kipindi ni saa moja (dakika 60). Katika miaka yote miwili wanachuo watasoma mihula 4. Muhula I utakuwa miezi 5 kwa kila mwaka na muhula II kwa kila mwaka utakuwa miezi 3. Muhula II kwa kila mwaka wanachuo watafanya mazoezi ya ufundishaji (BTP) katika shule za msingi watakazopangiwa kwa mafunzo hayo.

**Upimaji**

Muhtasari huu unatoa mapendekezo ya mbinu za upimaji ambazo zitamwezesha mkufunzi kuona kama malengo mahususi yanafikiwa. Mwanafunzi atapimwa kwa kutumia zana au mbinu mbalimbali. Mfano: majaribio, kazi mradi, mkoba wa kazi, kazi binafsi, mitihani ya mwisho wa

muhula na mwisho wa kozi. Alama za mazoezi endelevu ni asilimia 50% na Mtihani wa mwisho wa kozi ni asilimia 50%. Alama za mazoezi ya ufundishaji wa muda mrefu zitajitegemea na utaratibu wa upimaji utatolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Jedwali la Mchanganuo wa Upimaji Endelevu na Tamati.

| **Na.** | **Vipengele** | **Mbinu za Upimaji** | **Mwaka 1** | | **Mwaka 2** | | **Idadi ya Marudio** | **Alama %** | **Jumla %** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Muhula 1** | **Muhula II** | **Muhula 1** | **Muhula II** | | | |
| 1 | Taaluma | i) Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 05 | 25 |
| | | ii)Kazi mradi | - | 1 | 1 | - | 2 | 05 | |
| | | iii) Kazi za kimaandishi (Insha) | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 05 | |
| | | iv) Mtihani wa Muhula | 1 | 1 | 1 | 1 | 3 | 10 | |
| 2 | Ufundishaji | i) Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 05 | 25 |
| | | ii) Mkoba wa kazi | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 05 | |
| | | iii) Kazi za kimaandishi (Insha) | 1 | 1 | 1 | - | 3 | 05 | |
| | | iv) Mtihani wa Muhula | 1 | 1 | 1 | - | - | 10 | |
| | | v) Mtihani wa Taifa (Taaluma na Ufundishaji | | | | 1 | 1 | 50 | 50 |
| | JUMLA | | | | | - | - | 100 | 100 |

## SEHEMU A: TAALUMA YA HISTORIA

### Madhumuni ya Kufundisha Taaluma ya Somo la Historia

Madhumuni ya kufundishia taaluma ya historia ni kuwezesha wanachuo:

a) Kuelewa asili ya binadamu, mabadiliko yake kimaumbile, pamoja na hatua alizopiga katika maendeleo ya sayansi na teknolojia.
b) Kufahamu sababu na athari za uvamizi, utawala na uchumi wa kikoloni; sababu na hatua zilizochukuliwa na Waafrika kudai uhuru na hatua za maendeleo walizopiga hadi sasa.

### Ujuzi katika Taaluma ya Somo la Historia

Baada ya kusoma Historia katika mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti, wanachuo wanatarajiwa kuonyesha ujuzi ufuatao:

a) Kuchanganua taarifa za chimbuko la binadamu na hatua za maendeleo yake kimaumbile, kiuchumi na kijamii katika zama za mawe na zama za chuma.
b) Kutafuta taarifa za chimbuko, mahusiano ya kijamii na maendeleo ya koo na vyuo vyao.
c) Kutafuta, kuchambua na kutathmini taarifa za kihistoria juu ya sababu na athari za uvamizi wa kikoloni Tanzania na bara la Afrika na jitihada zilizofanywa na Waafrika kupinga uvamizi wa kikoloni.
d) Kutafuta na kutafsiri kiyakinifu sababu, mbinu na mikakati iliyotumiwa na mabeberu kuanzisha tawala za kikoloni na uchumi wa kikoloni katika Afrika.
e) Kutafuta, kuchambua na kutafsiri sababu, mbinu na mikakati iliyotumiwa na waafrika kudai uhuru na hatua zilizochukuliwa na Waafrika kuleta maendeleo baada ya uhuru.
f) Kujenga na kuonyesha ujuzi/uwezo wa kufundisha/kujifunza masomo ya sayansi, hisabati na lugha.

### Malengo ya Somo la Historia

Baada ya kusoma somo la Historia katika mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti wanachuo wanatarajiwa waweze:

a) Kufahamu chimbuko la koo zao na vyuo vyao na mahusiano ya kijamii katika koo na chuo.
b) Kuelewa hatua za maendeleo katika koo na vyuo vyao pamoja na kukusanya taarifa za kihistoria za koo na vyuo vyao.

c) Kufahamu chimbuko la binadamu, mabadiliko yake kimaumbile na hatua za maendeleo yake kijamii, kiuchumi na kiteknolojia katika nyakati mbalimbali.
d) Kuelewa sababu na athari za uvamizi wa kikoloni Tanzania na Bara la Afrika na jitihada zilizofanywa na Waafrika kupinga uvamizi wa kikoloni.
e) Kutambua sababu, mbinu na mikakati iliyotumiwa na mabeberu kuanzisha tawala za kikoloni na uchumi wa kikoloni katika Afrika.
f) Kuelewa sababu, mbinu na mikakati iliyotumiwa na Waafrika kudai uhuru na hatua zilizochukuliwa na Waafrika kuleta maendeleo baada ya uhuru.

## 1.0 UKOO WETU

### 1.1 Dhana ya Ukoo na Chimbuko la Ukoo

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya ukoo.
b) Kutaja jina la ukoo wake na familia zenye uhusiano wa damu zinazounda ukoo wake.
c) Kueleza chimbuko au asili ya ukoo wake.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo katika kueleza dhana ya ukoo.
b) Maswali na majibu.
c) Utafiti binafsi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Picha za familia.
b) Mchoro mguso.
c) Mchoro wa mti wa ukoo
d) Orodha ya maswali.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Mazoezi ya uchoraji wa mti wa ukoo.
c) Mazoezi juu ya kufanya utafiti binafsi.

### 1.2 Mahusiano baina ya Wanaukoo

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuainisha shughuli zilizofanywa na wanaukoo hapo zamani.
b) Kutofautisha shughuli za kijamii zilizofanywa na wanaukoo hapo zamani na siku hizi.
c) Kutaja viongozi wa ukoo wake na kazi zao.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo kupata shughuli za wanaukoo hapo zamani.
b) Majadiliano ya vikundi.
c) Usomaji bainifu kwa minajili ya kupata taarifa mahsusi.
d) Kualika mgeni mwenye ujuzi.
e) Kukusanya taarifa kwa njia mbalimbali.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Taarifa za utafiti.
b) Taarifa za utafiti katika breili kwa wasioona.
c) Maandiko ya taarifa za mahusiano.
d) Maandiko ya taarifa za mahusiano baina ya wanaukoo katika breili kwa wasioona.
e) Michoro, picha na mabango vinavyoonyesha mahusiano baina ya wanaukoo.
f) Kadi yenye orodha ya maswali.
g) Redio, Kanda za Kaseti, CD na DVD zenye taarifa mbalimbali.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya darasani.
b) Mazoezi kuhusu majina ya viongozi wa ukoo wake na kazi zao
c) Majaribio kuhusu kutofautisha shughuli za kijamii.
d) Maswali ya utafiti.
e) Mazoezi ya uchoraji/utengenezaji wa michoro, picha na mabango.

## 2.0 CHUO CHETU

### 2.1 Historia na Uongozi wa Chuo Chetu Tangu Kilipoanzishwa

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza historia ya chuo chake.
b) Kutaja wakuu wa chuo na viongozi wakuu wa wanachuo na muda wao wa uongozi tangu chuo kilipoanzishwa.
c) Kuainisha majukumu ya mkuu wa chuo na majukumu ya kiongozi mkuu wa wanachuo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Utafiti kwa kusoma rekodi.
b) Kufanya usaili.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Taarifa za utafiti.
b) Taarifa za utafiti katika breili kwa wasioona.
c) Mabango, picha na chati zinazoonesha orodha ya wakuu wa chuo na viongozi wakuu wa wanachuo.
d) Maandiko yenye taarifa (gazeti la chuo) tangu chuo kilipoanzishwa.
e) Maandiko yenye taarifa (gazeti la chuo) tangu chuo kilipoanzishwa katika breili kwa wasioona.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mazoezi ya uchoraji wa chati.

### 2.2 Maendeleo, Matatizo na Matarajio ya Chuo tangu Kilipoanzishwa

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza mafanikio na matatizo ya chuo tangu kilipoanzishwa.
b) Kueleza matarajio ya chuo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kufanya utafiti.
b) Kualika mgeni.
c) Majadiliano katika vikundi na uwasilishaji.
d) Mdahalo.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Kadi yenye orodha ya maswali kuhusu maendeleo, matatizo na matarajio ya chuo tangu kilipoanzishwa.
b) Kadi yenye orodha ya maswali katika breili kwa wasioona.
c) Maandiko.
d) Maandiko katika breili kwa wasioona.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mazoezi ya kuchora chati ya uongozi katika chuo.
c) Chemsha bongo.

## 3.0 ASILI NA MABADILIKO YA BINADAMU, TEKNOLOJIA NA MAZINGIRA

### 3.1 Asili na Mabadiliko ya Kimaumbile ya Binadamu

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuchambua maelezo ya kimila, kidini na kisayansi kuhusu asili ya binadamu.
b) Kuonyesha uhusiano baina ya maelezo ya kidini na kisayansi kuhusu asili ya binadamu.
c) Kueleza mabadiliko ya kimaumbile ya binadamu hatua kwa hatua.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano ya vikundi.
b) Usomaji bainifu wa maandiko anuai.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Orodha ya maswali.
b) Orodha ya maswali katika breili kwa wasioona katika karatasi za kawaida.
c) Maandiko kuhusu asili na mabadiliko ya kimaumbile ya binadamu.
d) Picha/michoro.
e) Picha/michoro mguso inayoonesha hatua za mabadiliko ya maumbile ya binadamu katika breili kwa wasioona.
f) CD, DVD au Kanda za Video.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Maswali ya insha.
c) Mazoezi.
d) Majaribio.
e) Utafiti, Kazi mradi.

## 3.2 Binadamu Wakati wa Zama za Mawe

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuchambua aina ya zana alizobuni binadamu
b) Kueleza ubora wa zana na jinsi zilivyotumiwa katika zama za mawe za kale, zama za mawe za kati na zama za mawe za mwisho.
c) Kuelezea udhaifu wa zana wakati wa zama za mawe.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu.
b) Kuchunguza.
c) Kuchunguza mabaki ya michoro/picha zinazoonesha matumizi ya zana za mawe na kuzijadili.
d) Kutengeneza mifano ya zana za mawe.
e) Kuandaa kumbukumbu za ripoti binafsi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Mabaki ya zana za zama za mawe.
b) Michoro ya zana za zama za mawe.
c) Picha za zana za mawe katika nyakati mbalimbali.
d) Maandiko kuhusu zana za zama za mawe.
e) Picha za shughuli mbalimbali za watu wa kale.
f) Maandiko kuhusu zama za mawe katika breili kwa wasioona.
g) Michoro/picha mguso za zana za mawe katika nyakati mbalimbali kwa wasioona.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mazoezi ya uchoraji wa picha/michoro ya zana za mawe.
c) Majaribio.
d) Fomu ya mlinganisho wa viwango.

## 3.3 Binadamu katika Zama za Chuma

**Muda:** Saa 7

**Malengo mahususi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuchambua aina ya zana zilizobuniwa katika zama za chuma.
b) Kueleza ubora na mapungufu ya zana za chuma wakati wa kuzitumia hapo kale.
c) Kutofautisha shughuli za binadamu wa zama za chuma na wakati wa zama za mawe.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu.
b) Kuchunguza michoro na picha za zana za chuma.
c) Kuchunguza mabaki ya zana za zama za chuma na kuzijadili.
d) Kuchora ramani ya Afrika.

**Zana/Vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Mabaki ya zana za chuma za zama za chuma.
b) Michoro ya zana za chuma za zama za chuma.
c) Picha za zana za chuma za zama za chuma
d) Maandiko kuhusu zana za zama za chuma .
e) Maandiko kuhusu zana za chuma katika breili kwa wasioona.
f) Michoro/picha mguso za zana za zama za chuma kwa wasioona.
g) Ramani ya Afrika inayoonesha sehemu maalum kulikovumbuliwa zana za chuma.

**Upimaji.**

a) Maswali ya insha.
b) Mazoezi ya uchoraji wa picha/michoro.
c) Majaribio.
d) Chemsha bongo.

## 4.0 VITANGULIZI VYA UKOLONI TANGANYIKA, ZANZIBAR NA KWINGINEKO AFRIKA

### 4.1 Makundi, Malengo na Majukumu ya Vitangulizi vya Ukoloni.

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuainisha makundi na malengo ya vitangulizi vya ukoloni.
b) Kujadili namna vitangulizi vya ukoloni vilivyotekeleza majukumu yao.
c) Kubainisha maeneo yaliyofikiwa na vitangulizi vya ukoloni.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu wa maandiko.
b) Majadiliano.
c) Matumizi ya picha.
d) Matumizi ya ramani ya Africa.
e) Kutembelea tovuti zinazohusu vitangulizi vya ukoloni.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko
b) Ramani ya Afrika
c) Maandiko katika breili kwa wasioona
d) CD, DVD na Kaseti za Video.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mazoezi ya kuchora ramani ya Afrika
c) Majaribio, chemsha bongo.

## 4.2 Uvamizi na Kugawanywa kwa Bara la Afrika

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza sababu za mataifa ya Ulaya kuivamia na kuigawa Afrika.
b) Kuchambua mataifa yaliyohusika na uvamizi na kugawanywa kwa bara la Africa.
c) Kuchambua matokeo ya uvamizi na kugawanywa kwa Afrika.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kualika mgeni.
b) Usomaji bainifu.
c) Majadiliano.
d) Matumizi ya mtandao (internet).

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko katika breili kwa wasioona.
c) Ramani ya Afrika.

d) Mtandao.

**Upimaji**

a) Majaribio juu ya sababu za uvamizi na matokeo ya kugawanywa kwa bara la Afrika.
b) Mazoezi ya uchoraji wa ramani ya Afrika kuonesha namna Afrika ilivyogawanywa.
c) Fomu ya ulinganisho wa viwango.

## 5.0 UPINZANI DHIDI YA UVAMIZI WA KIKOLONI AFRIKA

### 5.1 Mapambano ya Awali Dhidi ya Ukoloni Afrika.

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuchanganua sababu za upinzani dhidi ya ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika.
b) Kuelezea mbinu zilizotumika kupambana na uvamizi wa kikoloni Africa.
c) Kuchambua matokeo ya mapambano ya awali dhidi ya ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu wa maandiko.
b) Majadiliano.
c) Mikataba ya kazi binafsi, kumbukumbu za ripoti binafsi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko katika breili kwa wasioona.
c) Ramani za maeneo mbalimbali ya Afrika zinazoonesha baadhi ya jamii zilizopambana na wavamizi wa kibeberu.
d) Ramani mguso.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya uchoraji wa ramani.
b) Maswali ya insha.
c) Ripoti, Orodha hakiki.

## 6.0 UTAWALA NA UCHUMI WA KIKOLONI AFRIKA

### 6.1 Uanzishaji wa Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza sababu za kuanzisha tawala za kikoloni Afrika na aina zake.
b) Kuchambua sababu za kuanzisha uchumi wa kikoloni Afrika na aina zake.
c) Kuelezea aina za uchumi wa kikoloni ulioanzishwa Africa.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kualika mgeni.
b) Kufanya utafiti wa kimaktaba.
c) Majadiliano.
d) Utafiti, Kazi mradi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko katika breili kwa wasioona.
c) CD, DVD na Kanda za video.

**Upimaji**

a) Mazoezi.
b) Majaribio.
c) Ripoti za utafiti na kazi mradi.

## 6.2 Athari za Kuanzishwa kwa Tawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kujadili athari za kuanzishwa kwa tawala za kikoloni Afrika.

b) Kujadili athari za kuanzishwa kwa uchumi wa kikoloni Afrika.

**Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia**

a) Kufanya utafiti wa kimakitaba.

b) Majadiliano.

c) Majadiliano/mdahalo juu ya athari za tawala na uchumi wa kikoloni.

d) Kukusanya taarifa kwa njia ya redio, mtandao na magazeti.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko kuhusu athari za kuanzishwa kwa utawala na uchumi wa kikoloni Afrika.

b) Maandiko katika breili kwa wasioona.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi mafupi.

b) Majaribio.

c) Chemsha bongo.

# 7.0 UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

## 7.1 Harakati za Kupigania Uhuru

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Chanzo cha harakati za kupigania uhuru barani Afrika.

b) Kujadili mbinu na mikakati iliyotumika kudai uhuru katika makoloni mbalimbali ya Afrika.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kufanya utafiti wa maktaba.
b) Mdahalo.
c) Majadiliano ya vikundi.
d) Matembezi ya galari.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko katika breili kwa wasioona.
c) Mtandao CD, DVD na Kanda za Video.
d) Picha za baadhi ya wanaharakati waliodai uhuru Afrika.

**Upimaji**

a) Mazoezi ya kiinsha.
b) Mazoezi ya kuchora ramani ya Afrika kuonesha baadhi ya sehemu ambazo mapambano ya kivita yaliendeshwa wakati wa kudai uhuru Afrika.

## 7.2 Kupatikana kwa Uhuru katika Makoloni Mbalimbali ya Afrika

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kubainisha makoloni mbalimbali na nchi za Afrika walizozitawala.
b) Kuchanganua nchi zilizotumia mapinduzi ya kijeshi katika kupata uhuru.
c) Kuelezea sababu za kutofautiana kwa taratibu zilizotumika katika kupata uhuru katika makoloni mbalimbali ya Afrika.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu wa maandiko.
b) Kualika mtaalam.
c) Matumizi ya mtandao, CD, DVD na Kanda za Video.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko katika breili kwa wasioona.
c) Mtandao, CD na DVD.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mtihani/majaribio kuhusu taratibu zilizotumika kupata uhuru Afrika.

## 8.0 MABADILIKO YA KIJAMII, KISIASA NA KIUCHUMI KATIKA AFRIKA HURU

### 8.1 Mabadiliko ya Kijamii

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuanisha huduma za kijamii baada ya uhuru katika Afrika.
b) Kuelezea sababu za kuanzishwa kwa huduma mbalimbali za kijamii wakati wa ukoloni.
c) Kutathmini mafanikio na mapungufu ya upatikanaji wa huduma za jamii katika Afrika huru.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu wa maandiko.
b) Majadiliano.
c) Kualika mgeni.
d) Matumizi ya mtandao/tovuti.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Chati inayoonesha orodha ya mafanikio na mapungufu ya upatikanaji wa huduma za jamii katika Afrika huru.
b) Maandiko/makala.
c) Makala/maandiko katika breili.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mtihani/majaribio.
c) Chemsha bongo.

## 8.2 Mabadiliko ya Kisiasa

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuelezea mabadiliko ya kisiasa baada ya uhuru katika nchi za Afrika.
b) Kufafanua chanzo/migogoro ya kisiasa katika nchi za Afrika.
c) Kutathmini mafanikio na mapungufu katika mabadiliko ya kisiasa katika Afrika huru.
d) Kuanisha madhara ya migogoro

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kualika mgeni (mwanahistoria, mwalimu, mwanasiasa).
b) Usomaji bainifu wa maandiko.
c) Bungua bongo, majadiliano kwa njia ya vikundi na uwasilishaji.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Makala/maandiko.
b) Makala/maandiko katika breile kwa wasioona.
c) Chati inayoonesha kwa ufupi orodha ya mafanikio na mapungufu ya kisiasa katika Afrika huru.
d) Chati mguso.

**Upimaji**

a) Majaribio.
b) Maswali mafupi.
c) Mkusanyiko wa kazi alizofanya mwanachuo.

## 8.3 Mabadiliko ya Kiuchumi

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuanisha mabadiliko ya kiuchumi baada ya uhuru katika Afrika.
b) Kutathmini mafanikio na mapungufu ya kiuchumi katika Afrika huru.
c) Kuelezea mchango wa mabadiliko chanya ya kiuchumi katika maendeleo ya baadhi ya nchi za Afrika huru.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Utafiti katika maktaba.
b) Majadiliano katika makundi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Makala/maandiko.
b) Makala/maandiko katika breili kwa wasioona.
d) Chati.
e) Chati mguso.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mazoezi ya darasani.

# 9.0 USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

## 9.1 Jumuiya ya Afrika Mashariki

**Muda:** Saa 6

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza malengo ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
b) Kutathmini mafanikio, matatizo na matarajio ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
c) Kuelezea sababu za kutaka kurudisha/kufufua jumuiya hiyo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Usomaji bainifu wa maandiko kupata taarifa.
c) Majadiliano juu ya malengo ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
d) Kutembelea taasisi husika ili kukusanya taarifa na kufanya mawasilisho.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko ya breili kwa wasioona.
c) Ramani inayoonesha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
d) Ramani mguso inayoonesha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa wasioona.
e) Mtandao/tovuti.

**Upimaji**

a) Uchoraji wa ramani inayoonesha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
b) Majaribio.
c) Ripoti za utafiti.

### 9.2 Umoja wa Afrika

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza malengo ya kuundwa kwa Umoja wa Afrika na matarajio ya umoja huo.
b) Kutathmini mafanikio, matatizo na matarajio ya Umoja wa Afrika.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Utafiti wa kimaktaba.
b) Usomaji bainifu kupata taarifa.
c) Mdahalo kuhusu mafaniko, matatizo na matarajio ya Umoja wa Afrika.

d) Kutembelea mtandao/tovuti na kukusanya taarifa na kufanya mawasilisho.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko ya breili kwa wasioona.
c) Ramani inayoonesha nchi wanachama wa Umoja wa Afrika.
d) CD, DVD na Kanda za Video.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi kuhusu malengo ya kuundwa, mafanikio, matatizo na matarajio ya Umoja wa Afrika.
b) Majaribio.
c) Ripoti za utafiti na kazi mradi.

### 9.3 Umoja wa Mataifa

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza malengo ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa.
b) Kutathmini mafanikio, matatizo na matarajio ya Umoja wa Mataifa na Mashirika yake.
c) Kuanisha mchango wa mashirika ya Umoja wa mataifa kwa nchi mbalimbali wanachama.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu.
b) Matembezi ya galari kuhusu malengo ya kuundwa kwa Umoja wa Mataifa.
c) Majadiliano
d) Utafiti, kazi mradi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko
b) Maandiko ya breili kwa wasioona kuhusu malengo ya kuundwa, mafanikio, matatizo na matarajio ya Umoja wa Mataifa.
c) Ramani ya ukutani inayoonyesha nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa.
d) Ramani mguso.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Mitihani/majaribio.
c) Ripoti za utafiti.

## SEHEMU YA PILI: UFUNDISHAJI WA SOMO LA HISTORIA

**Madhumuni ya Kufundisha Ufundishaji wa Somo la Historia**

Madhumuni ya kufundisha ufundishaji wa somo la Historia kwa wanachuo ni:

a) Kuwajengea uwezo wa kutumia njia/mbinu shirikishi katika kufundisha somo la Historia.
b) Kuwajengea uwezo wa kutafuta, kutafsiri na kutumia taarifa za kihistoria kwa ajili ya kujiongezea maarifa na uwezo mpana wa kufundisha somo la Historia.
c) Kuwaandaa kwa ajili ya kufundisha somo la Historia katika shule za msingi kwa kuchopeka masuala mtambuko na kuzingatia elimu jumuishi.

**Ujuzi katika kufundisha ufundishaji wa Somo la Historia**

Ujuzi unaotarajiwa kujengwa na wanachuo katika somo la Historia ni:

a) Kuchambua na kutumia vifaa/zana za kufundishia/kujifunzia.
b) Kuchagua na kupangilia njia/mbinu na zana za kufundishia/kujifunzia ili kufanikisha ufundishaji/ujifunzaji wa somo la Historia.
c) Kubuni, kufaragua na kutengeneza zana za kufundishia/kujifunzia somo la Historia.
d) Kufanya maandalizi sahihi ya kufundishia kwa kuandaa Azimio la Kazi, Andalio la Somo, nukuu za somo na maswali.
e) Kukuza stadi za kihistoria za wanafunzi, kuchopeka masuala mtambuko katika maudhui ya somo na kufundisha somo katika mazingira ya elimu jumuishi.
f) Kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi katika somo la Historia na kuchukua hatua zinazostahili

**Malengo ya kufundisha ufundishaji wa Somo la Historia**

Malengo ya kufundisha ufundishaji wa somo la Historia ngazi ya cheti ni kuwawezesha wanachuo waweze:

a) Kuchambua na kutumia muhtasari wa somo la Historia kwa shule za msingi na uwezo wa maandiko mengine ya kufundishia/kujifunzia.
b) Kutafuta, kuchambua na kutumia taarifa za kihistoria ili kujiongezea maarifa na uwezo mpana wa kufundisha.
c) Kutumia njia/mbinu shirikishi katika kufundisha somo la Historia.

d) Kubuni, kufaragua na kutengeneza zana za kufundishia/kujifunzia kwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira ya shule.
f) Kuandaa Azimio la Kazi, Andalio la Somo na nukuu za somo kwa ajili ya kufundishia somo la Historia.
g) Kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi katika somo la Historia na kuchukua hatua zinazostahili ili kuboresha ufundishaji/ujifunzaji.
h) Kubaini matatizo binafsi ya wanafunzi ya kujifunza somo la Historia na kufundisha Historia katika mazingira ya elimu jumuishi.

.

## 1.0 MISINGI YA UFUNDISHAJI/UJIFUNZAJI WA SOMO LA HISTORIA

### 1.1 Kufundisha/Kujifunza kwa Vitendo

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasiri maana ya msingi wa kufundisha na kujifunza kwa vitendo.
b) Kuonesha namna ya kufundisha na kujifunza kwa vitendo.
c) Kuelezea jinsi ujifunzaji/ufundishaji kwa vitendo unavyofanikisha ufundishaji/ujifunzaji wa somo la Historia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu wa maandiko.
b) Majadiliano.
c) Matumizi ya kaseti za redio au luninga.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Maandiko ya breili kwa wasioona.
c) Orodha ya maswali .
d) Kaseti za redio, luninga.

**Upimaji**

a) Maswali ya insha.
b) Majaribio.

### 1.2 Kukuza Uwezo wa Kudadisi na Kufikiri Kiyakinifu.

**Muda:** Saa 8

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza namna ufundishaji/ujifunzaji wa somo la Historia unavyoweza kukuza uwezo wa kudadisi na kufikiri kiyakinifu.

b) Kueleza jinsi atakavyowawezesha wanafunzi kudadisi na kufikiri kiyakinifu katika kufundisha somo la Historia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano.
b) Visa mafunzo.
c) Usomaji bainifu wa maandiko.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko, vitabu vya somo la Historia.
b) Maandiko katika breili kwa wasioona.
c) Matini ya misingi ya kufundishia somo la Historia.

**Upimaji**

a) Orodha ya maswali.
b) Majaribio.
c) Chemsha bongo.

## 1.3 Kutumia Dhana, Maarifa na Stadi za Kihistoria Katika Maisha ya Kila Siku.

**Muda:** Saa 8

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufafanua dhana, maarifa na stadi za kihistoria.
b) Kuelezea umuhimu wa kutumia dhana, maarifa na stadi za kihistoria katika kufundisha somo la Historia.
c) Kueleza jinsi dhana, maarifa na stadi za kihistoria zinavyoweza kutumiwa katika maisha ya kila siku.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Fikiri-Jozisha na Jadili.
b) Kutembelea mtandao/tovuti ili kukusanya taarifa na kufanya mawasilisho.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.

b) Maandiko katika breili kwa wasioona.

c) Mtandao/tovuti.

d) Matini ya misingi ya kufundisha somo la Historia.

**Upimaji**

a) Fomu ya mlinganisho wa viwango.

b) Fomu ya uchunguzi.

c) Maswali ya insha .

## 2.0 UCHAMBUZI WA VIFAA/ZANA ZA KUFUNDISHIA/KUJIFUNZIA

**2.1** **S**ifa za Muhtasari Sanifu wa Somo la Historia

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufafanua vipengele vinavyounda muhtasari wa somo la Historia.

b) Kutathmini sifa za muhtasari bora wa somo la Historia.

c) Kuchambua muhtasari Sanifu wa Somo la Historia. (kuzingatia mwonekano wa nje na mpangili wa ndani, maarifa, stadi na mwelekeo, mbinu za upimaji na tathmini).

d) Kueleza umuhimu wa kuchambua muhtasari wa somo la Historia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Uchunguzi na majadiliano.

b) Maswali na majibu.

c) Usomaji bainifu.

d) Majadiliano.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Muhtasari wa Somo la Historia kwa Shule za Msingi Darasa III – VII (2006).
b) Muhtasari wa Mafunzo ya ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya msingi Somo la Historia.

**Upimaji**

Mazoezi kuhusu sifa za muhtasari bora. Chemsha bongo na majaribio.

## 2.2 Sifa za Kitabu cha Kiada Bora cha Somo la Historia

**Muda:** Saa 8

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuelezea maana ya kitabu bora cha kiada.
b) Kutathmini sifa za kitabu bora cha kiada cha somo la Historia.
c) Kuchambua kitabu bora cha kiada cha somo la Historia.
d) Kuonesha uhusiano kati ya Muhtasari wa somo na kitabu cha kiada.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Uchunguzi na majadiliano.
b) Maswali na majibu.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Sampuli za vitabu vya kiada vya Historia kwa Shule za Msingi Darasa III – VII.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi mafupi.
b) Mazoezi .

## 2.3 Sifa za Kiongozi cha Mwalimu Sanifu cha Somo la Historia

**Muda:** Saa 8

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuelezea umuhimu wa kiongozi cha mwalimu.
b) Kutathmini sifa za kiongozi cha mwalimu bora cha somo la Historia.
c) Kulinganisha kati ya Muhtasari wa somo la Historia, Kitabu cha Kiada cha somo na Kiongozi cha mwalimu cha somo la Historia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Uchunguzi na majadiliano.
b) Maswali na majibu.
c) Uchunguzi wa kitabu cha kiada na kiongozi cha mwalimu.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli za nakala za Kiongozi cha Mwalimu cha Historia kwa Shule za Msingi Darasa III – VII.
b) Sampuli za nakala za vitabu vya kiada.

**Upimaji**

a) Mazoezi.
b) Majaribio kuhusu sifa za Kiongozi cha Mwalimu bora.
c) Maswali mafupi mafupi.

## 3.0 KUJIANDAA KWA AJILI YA KUFUNDISHA

## 3.1 Uandaaji wa Azimio la Kazi

**Muda:** Saa 8

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza uhusiano uliopo kati ya muhtasari wa somo la Historia na Azimio la Kazi.
b) Kuelezea vipengele muhimu vinavyounda Azimio la kazi.

c) Kuandaa Azimio la Kazi.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Uchunguzi
b) Maswali na majibu.
c) Kazi za vikundi vidogo kujadili na kuandika mfano wa Azimio la Kazi.
d) Majadiliano ya vikundi na mawasilisho.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Muhtasari wa Somo la Historia kwa Shule za Msingi Darasa la III – VII (2006).
b) Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi: Somo la Historia (2008).
c) Muundo rasmi wa Azimio la Kazi.
d) Muundo rasmi wa Azimio la Kazi katika breili kwa wasioona.
e) Orodha ya maswali ya kuendeshea majadiliano kuhusu vipengele vya Azimio la Kazi.
f) Vitabu vya rejea.

**Upimaji**

a) Fomu ya uchunguzi.
b) Mazoezi ya kuandaa Azimio la Kazi la darasa mojawapo la msingi.
c) Majaribio na mitihani ya mwisho wa muhula.

## 3.2 Uandaaji wa Andalio la Somo

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza uhusiano uliopo kati ya Azimio la Kazi na Andalio la Somo
b) Kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa Andalio la somo.
c) Kuandaa Andalio la Somo la Historia.
d) Kufanya ufundishaji kiduchu kwa kutumia andalio la somo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Uchunguzi na majadiliano.
b) Kazi ya vikundi kuandaa na kujadili Andalio la Somo.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Muhtasari wa Somo la Historia kwa Shule za Msingi Darasa la III – VII (2006).
b) Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi: Somo la Historia (2008).
c) Muundo rasmi wa Azimio la Kazi.
d) Muundo rasmi Azimio la Kazi katika breili kwa wasioona.
e) Azimio la Kazi la mfano.
f) Kitabu cha kiada cha Historia cha darasa lililolengwa katika Azimio la Kazi .
g) Kiongozi cha Mwalimu kwa darasa lililolengwa.
h) Orodha ya maswali ya kuendeshea majadiliano ya vipengele vya Andalio la Somo.

**Upimaji**

a) Fomu ya uchunguzi kwa kupima ukamilifu wa Andalio la Somo.
b) Mazoezi ya kuandaa Andalio la Somo.
c) Majaribio kuhusu uandaaji wa Andalio la Somo.
d) Mitihani ya mwisho wa muhula .

### 3.3 Uandaaji wa Nukuu za Somo la Historia

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa nukuu za somo.
b) Kufafanua mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa nukuu za somo la Historia.
c) Kuandaa nukuu za somo la Historia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kazi ya vikundi kuandaa mfano wa nukuu za somo la Historia
b) Majadiliano.
c) Maswali na majibu.
d) Usomaji wa maandiko.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Andalio la somo la mfano lililotayarishwa hapo juu.
b) Muhtasari wa somo la Historia kwa Shule za Msingi Darasa la III – VII (2006).
c) Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi: Somo la Historia (2008).
d) Kitabu cha kiada cha Historia cha darasa lililolengwa.
e) Vitabu vya rejea vinavyohusiana na mada inayofundishwa.

**Upimaji**

a) Fomu ya uchunguzi wa kazi za vikundi
b) Majaribio kuhusu uandaaji wa nukuu za somo.

## 3.4 Shajara

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu na matumizi ya shajara katika ufundishaji/ujifunzaji wa somo la Historia.
b) Kufanya majaribio ya mfano wa kutumia shajara.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu.
b) Maswali na majibu
c) Kazi za vikundi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli au mfano wa shajara
b) Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi: Somo la Historia (2008).
c) Muhtasari wa somo la historia kwa shule za Msingi Darasa la III – VII (2006).
d) Maandiko anuai yanayohusu shajara.

**Upimaji**

a) Fomu ya uchunguzi ya kazi za mwanachuo
b) Mitihani
c) Majaribio kuhusu shajara na matumizi yake.

### 3.5 Kuchagua, Kufaragua na Kutengeneza Vifaa/Zana za Kufundishia/Kujifunzia

**Muda:** Saa 9

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuchagua vifaa/zana bora na sahihi za kufundishia/kujifunzia somo la Historia.
b) Kufaragua vifaa/zana bora na sahihi za kufundishia/kujifunzia somo la Historia.
c) Kutengeneza vifaa/zana bora na sahihi za kufundishia/kujifunzia somo la Historia.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

Majadiliano ya darasa juu ya vigezo vya kuzingatia

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Muhtasari wa somo la Historia kwa Shule za Msingi Darasa la III–VII (2006).
b) Makunzi na vyombo vya kutengenezea zana.
c) Azimio la Kazi la somo kwa darasa husika.

**Upimaji**

a) Fomu ya uchunguzi wa kazi za mwanachuo
b) Orodha hakiki
c) Fomu ya uchunguzi wa kazi za vikundi
d) Mtihani na majaribio.

## 3.6 Maandalizi na Mipango ya Mazoezi ya Ufundishaji (B.T.P)

**Muda:** Saa 9

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza kwa ufasaha maandalizi na mipango ya mazoezi ya ufundishaji.
b) Kuchanganua namna ya kupata, kuandaa, kutengeneza na kukusanya vifaa/zana muhimu zinazohitajika kutumika wakati wa mazoezi ya ufundishaji.
c) Kueleza umuhimu wa kutafakari juu ya utendaji wake wakati wote atakapokuwa kwenye mazoezi ya ufundishaji.
d) Kufafanua vipengele muhimu vya kuzingatia wakati wa kuandika ripoti ya mazoezi ya ufundishaji.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano.
c) Majadiliano juu ya umuhimu wa kutafakari juu ya utendaji wa mazoezi ya ufundishaji.
d) Matumizi ya CD, DVD na Kanda za Video.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko kuhusu namna ya kujiandaa kwa mazoezi ya ufundishaji.
b) Maandiko kuhusu namna ya kujiandaa kwa mazoezi ya ufundishaji.
c) Muhtasari wa somo la Historia kwa Shule za Msingi (2006)
d) Makunzi anuai ya kutengenezea zana za kufundishia/kujifunzia.
e) Vyombo au vifaa vya kutengenezea zana za kufundishia.
f) CD, DVD na Kanda za Video.

**Upimaji**

a) Fomu ya kuchunguza au kuhakiki utengenezaji wa zana na ufaraguzi wa zana.
b) Mazoezi na majaribio kuhusu ubunifu, utengenezaji, ufaraguzi na upatikanaji wa zana.
c) Mitihani ya mwisho wa muhula
d) Mtihani na majaribio.
e) Utayarishaji wa ripoti ya mazoezi ya ufundishaji

## 4.0 UFUNDISHAJI WA MADA ZA SOMO LA HISTORIA

### 4.1 Ukoo Wetu

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza namna atakavyotumia picha za familia mbalimbali zenye uhusiano wa damu kufundisha wanafunzi wake maana ya ukoo.
b) Kuonesha jinsi atakavyotumia maswali kuwaongoza wanafunzi wake kufanya utafiti juu ya:-
   i) Majina ya koo zao
   ii) Familia zinazounda koo zao
   iii) Asili ya koo zao.
d) Kuonesha jinsi atakavyoongoza wanafunzi wake kuwasilisha na kujadili matokeo ya utafiti wao.
e) Kufanya onesho mbinu juu ya ufundishaji wa mada hiyo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali
b) Majadiliano
c) Majadiliano kuhusu namna ya kuwaongoza wanafunzi kuwasilisha matokeo ya utafiti wao.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Picha za wanafamilia wenye uhusiano wa damu zinazounda ukoo.
b) Mchoro mguso.
c) Tafiti/kumbukumbu za ripoti/kazi mradi kuhusu ukoo wetu.

**Upimaji**

a) Fomu ya mlinganisho wa viwango kuhusu ukoo wetu.
b) Ripoti za utafiti na kazi mradi kuhusu ukoo wetu.
c) Maswali mafupi mafupi kuhusu ukoo wetu.

## 4.2 Asili na Mabadiliko ya Binadamu

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kubuni maswali atakayowapa wanafunzi wake kufanya utafiti juu ya maelezo ya kimila kuhusu asili ya binadamu na ayajadili na wanachuo wenzake.
b) Kuonesha jinsi atakavyowaongoza wanafunzi wake kuwasilisha na kujadili matokeo ya utafiti wao katika vikundi.
c) Kueleza namna atakavyotumia maelezo ya kidini na kisayansi kuhitimisha ufundishaji/ujifunzaji wa mada ya asili ya binadamu.
d) Kufundisha kiduchu kwa kutumia mbinu zilizopendekezwa kukamilisha malengo mahsusi.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali ya mfano kwa ajili ya kufanya utafiti.
b) Majadiliano.

c) Maswali ya mfano kuwaongoza kupata/kufahamu maelezo ya kidini na kisayansi kuhusu asili ya binadamu.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Orodha ya maswali kuhusu asili na mabadiliko ya binadamu.
b) Maandiko kuhusu asili na mabadiliko ya binadamu.
c) Maandiko katika breili kwa wasioona.
d) Orodha ya maswali katika breili kwa wasioona.
e) Picha zinazoonesha hatua za mabadiliko ya maumbile ya binadamu.
f) Picha mguso kwa wasioona zinazoonesha hatua za mabadiliko ya maumbile ya binadamu.

**Upimaji**

a) Maswali ya kiinsha.
b) Maswali ya majaribio.

## 5.0 UPIMAJI NA TATHMINI

### 5.1 Uandaaji wa Zana za Upimaji

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kujadili aina ya zana inayotakiwa kwa upimaji.
b) Kuandaa sampuli za zana za upimaji.
c) Kuwasilisha sampuli ya zana za upimaji kwa majadiliano.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Usomaji bainifu.
b) Uandaaji wa zana za upimaji za mfano.
c) Uwasilishaji na majadiliano .

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko.
b) Sampuli za zana za upimaji.

**Upimaji**

a) Uchunguzi kuhusu uandaaji wa zana za upimaji.
b) Mazoezi kuhusu uandaaji wa zana za upimaji.

## 5.2 Usahihishaji na Uwekaji wa Kumbukumbu za Matokeo ya Kazi za Wanafunzi

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kutayarisha mwongozo wa usahihishaji wa kazi za wanafunzi kulingana na zana za upimaji.
b) Kueleza jinsi ya kusahihisha kazi za wanafunzi kulingana na aina mbalimbali ya zana za upimaji na mwongozo wa usahihishaji.
c) Kueleza namna ya kuingiza alama za wanafunzi na kutunza kumbukumbu za matokeo ya kazi zao.
d) Kufanya zoezi la usahihishaji na uwekaji wa kumbukumbu za matokeo ya kazi za wanafunzi.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Utayarishaji wa mwongozo wa usahihishaji wa mfano.
b) Majadiliano katika vikundi.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko kuhusu usahihishaji wa kazi za wanafunzi.
b) Sampuli za mwongozo wa usahihishaji.
c) Sampuli za mwongozo.
d) Sampuli ya fomu za kutunza kumbukumbu za matokeo.
e) Sampuli ya fomu za kutunza kumbukumbu katika breili.
f) Fomu ya uchunguzi kuhusu kazi za wanafunzi.

**Upimaji**

a) Mazoezi.
b) Majaribio.
c) Vitendo vya usahihishaji wa kazi za wanafunzi.

## 5.3 Utumiaji wa Matokeo ya Kazi za Wanafunzi

**Muda:** Saa 7

**Malengo Mahsusi:**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kupanga matokeo ya wanafunzi kwa mtiririko unaokubalika.
b) Kueleza jinsi atakavyotumia matokeo ya kazi za wanafunzi kuboresha ufundishaji/ujifunzaji wa somo la Historia.
c) Kufanya onesho mbinu juu ya utumiaji wa matokeo ya kazi za wanafunzi.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano.
b) Maswali na majibu.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Maandiko kuhusu tathmini.
b) Sampuli za maswali ya mwongozo.
c) Mkoba wa kazi za wanafunzi.
d) Fomu ya mlinganisho wa viwango.

**Upimaji**

Mazoezi kuhusu utumiaji wa matokeo ya kazi za wanafunzi.

## REJEA ZILIZOTUMIKA

Angelo, A.T. et ali (1993); **Classroom Assessment Techniques, A Handbook for College Teachers**. San Fransisco; Tossey – Bass Publisher.

Brandes, D. et al; (1994); **A Guide to Student-Centred Learning**, Basil Blackwell LTD, Celtmeham, UK.

Kyriacon, C. (1997); **Effective Teaching in School: Theory and Practice**; Starley Theories Publishers LTD; Cheltenliam UK.

Lutatenekwa, F. (2008); **Kiongozi cha Mwalimu**. Dar es Salaam; Ben and Company Ltd.

Lutatenekwa, F. (2007); **Historia 3: Kiongozi cha Mwalimu**; Dar es Salaam: Ben and Company Ltd.

Shillington, K. (2004). **History of Africa**. Hong Kong: Macmillan Publishers.

Taasisi ya Elimu Tanzania; (2008): Framework for the Review of Certificate Teacher Education Curriculum (unpublished document).

Wizara ya Elimu na Utamaduni. (1996); **Muhtasari wa Maarifa ya Jamii kwa Shule za Msingi** Dar es Salaam: WyEMU.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (2003). Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti, Mbinu za Kufundishia Maarifa ya Jamii Dar es Salaam: WyEMU.

Illife, J. (1995) **Africans**: **The History of the Continent**, London, Cambridge University Press.

July, R.W. (1992) **A History of the African People**, Nairobi, East African Educational Publishers.

Lutatenekwa, F. (2007) **Historia 3, Kitabu cha Mwanafunzi**, Dar es Salaam, Ben and Company Ltd.

Lutatenekwa, F. (2008) **Historia 4, Kitabu cha Mwanafunzi**, Dar es Salaam, Ben and Company Ltd

Schimid, P.R. (`997) **Iron Technology in East Africa** London, Indiana University Press.

Shillington, K. (2004) **History of Africa**, Hong Kong Macmillan Publishers.